MKUSANYIKO WA TAARIFA ZA MWALIMU WA FAMILY DAY CARE 2

Maswali ya Kuuliza Huduma za Family Day Care

SWAHILI

Australian Government
Department of Education and Training

NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.

MKUSANYIKO WA TAARIFA ZA MWALIMU WA FAMILY DAY CARE:

Maswali ya Kuuliza Huduma za Family Day Care

Iwapo unafikiria kuwa, au umeombwa kuwa mwalimu wa Family Day Care, ni lazima ujisajili na huduma ya Family Day Care iliyoidhinishwa.

Walimu wa Family Day Care ni watu wanaotoa huduma za masomo ya utotoni yaliyoidhinishwa na kutunzia watoto wachanga nyumbani mwao.

Vituo vya huduma ya Family Day Care huwashirikisha walimu kama wafanyakazi au kama wakandarasi wa biashara ndogo ndogo kuwa sehemu ya huduma yao. Kituo cha huduma ndicho mtoa huduma za utunzaji wa watoto aliyeidhinishwa chini ya Sheria ya Kitaifa na Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani, ingawa walimu ndio wanaowatunza watoto.

Kuchagua ni huduma gani ya Family Day Care utakayojisajili nayo ni uamuzi muhimu - unahitaji kuhakikisha unajisajili na huduma unayoiamini na itakayotoa msaada na usaidizi unaohitaji.

Je, huduma za Family Day Care hufanya nini?

- Huhakikisha wewe ni mtu anayefaa kuelimisha na kutunza watoto.
- Hukagua nyumba yako kuhakikisha ni salama na ina ulinzi wa kutosha kwa watoto unaowatunza.
- Huwa na sera na taratibu unazoweza kufuata ili kusaidia kurahisisha kazi yako kama mwalimu na kuhakikisha unafanya unachohitajika kufanya kwa mujibu washeria.
- Huangalia kuhakikisha una bima, sifa stahiki na vyeti unavyohitaji kama mwalimu.
- Hukupa mafunzo ya jinsi ya kuanza unapoanza kazi kama mwalimu.
- Hukutembelea mara kwa mara ili kuhakikisha unawatunza watoto ipasavyo.
- Hukusaidia kuzidi kuimarisha ubora wa elimu na utunzaji unaotoa kwa watoto.
- Husimamia usaidizi wa ada ya utunzaji wa watoto wa Serikali ya Australia kwa niaba ya familia zinazostahiki unazotunzia watoto.
- Hutoza familia ada za kugharamia elimu na utunzaji unaotoa kwa watoto.
- Hulipa mishahara yako, au bili ikiwa unafanya kazi kwa misingi ya kandarasi.
- Huzidi kuendeleza taaluma yako (kupitia mafunzo).
- Muhimu zaidi, zinapaswa kuhakikisha unafuata Sheria na Kanuni za Kitaifa na unazingatia Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani kama mwalimu wa Family Day Care.

Je, unawezaje kupata huduma ya Family Day Care ambayo ni bora zaidi ya kujisajili nayo?

Kwa sababu kuna huduma kadhaa za Family Day Care unazoweza kujisajili nazo, unahitaji kuhakikisha unaridhishwa na ile unayochagua.

Ili kukusaidia kuchagua ile ambayo ni bora zaidi kwako, piga simu au tembelea kila huduma. Waulize maswali ili ujue jinsi wanavyoweza kukusaidia na wanachotarajia kutoka kwako kama mwalimu wa Family Day Care. Zungumza na walimu wengine ambao wamejisajili na huduma hiyo. Je, huduma hiyo ina sifa nzuri? Je, ni nini kadirio la ubora wa huduma hiyo? (Waulize au unaweza kuangalia mtandaoni katika www.startingblocks.gov.au/find-child-care)

Ni aina gani ya maswali unayopaswa kuuliza huduma za Family Day Care?

Maswali ya kukusaidia kuamua ni huduma gani ya Family Day Care unayopaswa kujisajili nayo:

- Je, uta**ajiriwa** na huduma hiyo au utakuwa **mkandarasi** wao?
- Je, ni ada na kodi gani wanazotoza walimu wao na familia wanazofanyia kazi?
- Je, ni walimu wangapi wamejisajili nao na wameajiri waratibu wangapi? (Waratibu ni wafanyakazi wa huduma watakaokusaidia kama mwalimu).
- Je, watakusaidia kupata sifa stahiki?
- Je, ni walimu wangapi wanaojiondoa kutoka kwa huduma hiyo? (Ikiwa walimu hukaa sana, hiyo ni dalili kuwa wameridhika na huduma hiyo ya Family Day Care.)
- Je, ni uendelezaji gani wa taaluma na usaidizi wanaotoa kwa walimu?
- Je, watakutembelea mara ngapi?
- Je, wanatoa huduma za ziada kama vile vikundi vya kucheza, ambapo unaweza kuleta watoto unaowatunza kucheza na watoto wengine?

HAKIKISHA WANAFUATA SHERIA!

Je, umealikwa na mtu yeyote kuwa mwalimu wa Family Day Care au kujisajili na huduma yao? Ni muhimu kufahamu unachokubali kufanya. Ikiwa huduma ya Family Day Care inavunja sheria au inajihusisha na ulaghai, unaweza kupatikana na hatia kama mmojawapo ya walimu wake. Hakikisha kuwa huduma yoyote ya Family Day Care unayojisajili nayo ni kweli, haivunji Sheria ya Kitaifa na inazingatia Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani.

Mambo muhimu

- Unapoanzisha biashara yako ya kutoa huduma za Family Day Care, ni lazima ujisajili na kituo kilichoidhinishwa cha huduma ya Family Day Care.
- Walimu wa Family Day Care hufanya kazi wakielekezwa na huduma ya Family Day Care.
- Wakati mwingine walimu hujiajiri lakini mara nyingine huajiriwa na kituo cha huduma.
- Huduma ya Family Day Care unayojisajili nayo ni mojawapo ya maamuzi muhimu zaidi utakayofanya unapoanzisha biashara yako ya Family Day Care. Ni muhimu kuuliza maswali mengi ili kuhakikisha umeridhika na huduma unayochagua.
- Huduma za Family Day Care zinapaswa kutoa usaidizi wa aina mbalimbali kwa walimu waliojisajili nao. Hii ni pamoja na mafunzo ya jinsi ya kuanza, masomo ya kujiendeleza kitaaluma na usaidizi wa kila mara.
- Baadhi ya huduma za Family Day Care zinaweza kutoa ada na malipo ya chini zaidi ya usimamizi lakini wasitoe usaidizi unaohitaji. Usijisajili na huduma ambayo ina ada za chini zaidi.
- Usijisajili na huduma ya Family Day Care ambayo unashuku inaweza kuwa inavunja Sheria ya Kitaifa au Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani. Hii inaweza kukuweka katika hatari ya kuvunja sheria pia.
- Njia bora zaidi ya kuhakikisha kuwa unapata msaada katika kazi yako kama mwalimu wa Family Day Care ni kwa kujisajili na huduma ya Family Day Care inayokusaidia na unayoiamini.

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

Je, ni lazima nijisajili na huduma ya Family Day Care?

Ndiyo. Ili kuwa mwalimu wa Family Day Care, ni lazima ujisajili na huduma ya Family Day Care iliyoidhinishwa.

Je, kuna aina tofauti za huduma za Family Day Care?

Ndiyo. Mengine ni mashirika yasiyo ya kibiashara. Zingine ni biashara. Zingine zinaendeshwa na serikali za mitaa au wahisani.

Je, ninawezaje kuamua ni huduma gani ninapaswa kujisajili nayo?

Zingatia mambo kama vile:

- Ni usaidizi gani watakupatia.
- Ni aina gani ya mafunzo wanayotoa wakati unapoanza.
- Ni ada au kodi gani wanazotoza walimu na familia.
- Ni usaidizi gani wa kujiendeleza kitaaluma/mafunzo wanaotoa.
- Watakutembelea mara ngapi.
- Ni nini kadirio la ubora wa huduma hiyo. (Unaweza kuangalia hili katika www.startingblocks.gov.au/find-child-care)
- Jinsi unavyofikiria wanafuata Sheria na Kanuni za Kitaifa na Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani kuhusu ruzuku za utunzaji wa watoto kutoka kwa Serikali wanazosimamia kwa niaba ya familia zinazostahiki.

LAINI YA KUTOA RIPOTI

Iwapo unashuku kuwa kuna ulaghai unaofanyika, unaweza kuwasiliana na Idara ya Elimu na Mafunzo ya Serikali ya Australia kupitia laini yao ya kuripoti na utoe maelezo mahususi kwa 1800 664 231 au utume barua pepe kwa tipoffline@education.gov.au. Unaweza kutoa ripoti bila kutaja jina lako iwapo unataka kufanya hivyo.

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA INAENDELEA

Je, ninawezaje kupata wapi huduma zaidi?

Ili kupata huduma zilizo karibu nawe, tembelea tovuti www.fdca.com.au na ubofye kichupo cha "find childcare".)

Je, ni nini ninapaswa kushuku?

Unapaswa kushuku iwapo unafikiri huduma inavunja Sheria ya Kitaifa na Sheria ya Usaidizi wa Nyumbani.

Unapaswa kushuku iwapo wanachokupa ni kizuri sana kuliko hali halisi.

Je, Family Day Care inadhibitiwa na sheria na kanuni gani?

Kuna sheria kadhaa zinazodhibiti jinsi huduma na walimu wa Family Day Care wanavyoendesha shughuli zao.

Sheri ambazo ni muhimu sana ni:

- Sheria ya Kitaifa ya Huduma za Elimu na Utunzaji www.acecqa.gov.au/national-law
- Kanuni za Kitaifa za Huduma za Elimu na Utunzaji www.acecqa.gov.au/national-regulations
- Sheria ya Usaidizi wa Familia: www.education.gov.au/family-assistance-law-0

FAHAMU MENGI ZAIDI

Umevutiwa? Fahamu mengi zaidi kwa kutembelea tovuti zifuatazo:

- **www.education.gov.au/compliance**
- **www.fdcsupport.org.au**
- **www.fdca.com.au**
- **www.acecqa.gov.au**

au kwa kuenda kwenye kituo cha huduma ya Family Day Care kilichopo karibu nawe. (Ili kupata kituo cha huduma hii kilicho karibu sana, tembelea tovuti **www.fdca.com.au** na kisha ubofye kichupo cha "find childcare".)

Australian Government
Department of Education and Training

since 1976
NSW FAMILY DAY CARE ASSOCIATION INC.